7. WAITING FOR THE BARBARIANS

7. WAITING FOR THE BARBARIANS

Vitabu100Siku100 na Kocha Dr Makirita Amani.

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha SABA kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.
WAITING FOR THE BARBARIANS ni riwaya iliyoandikwa na J. M. Coetzee inayohusu kuharibiwa kwa mji ulio mpakani kwa kisingizio cha kuwakabili maadui. Mji huo unaongozwa na hakimu anayesimamia sheria na haki na anapinga sana uvamizi unaopangwa, lakini anapingwa na kuteswa kwa misimamo yake. Uvamizi haufanikiwi, mji uliokuwa unastawi vizuri unaharibiwa kabisa.

👉1
Msimuliaji amempokea mgeni, ni Colonel Joll, kutoka jeshi la ulinzi. Ni mgeni muhimu hivyo anaandaliwa makazi mazuri.
Mgeni anamshangaza msimuliaji kwa miwani nyeusi aliyovaa, anasema inazuia mwanga wa jua usimsumbue.
Msimuliaji na wanajeshi wengine wamelala juu ya jengo.
Msimuliaji anaeleza hawana gereza la kuwaweka wafungwa, hivyo adhabu huwa ni kulipa faini na kazi za nje.
Anaelekeza wafungwa wawili walio kwenye chumba kidogo wawe kwenye mazingira safi, mgeni atapita kuwaangalia.
Anamtembeza mgeni kumwonesha maghala ya nafaka wanayolinda. Wanafika kwa wafungwa na kumweleza mgeni kwamba wafungwa hao wawili wamekamatwa siku mbili zilizopita, ambapo kuna uvamizi uliofanyika, japo wanakataa kuhusika na uvamizi huo.
Msimuliaji anamwambia mgeni anaweza kuwahoji kama anataka, atasaidia kutafsiri.
Msimuliaji anawauliza wafungwa maswali hawajibu.
Anamshawishi mfungwa mzee kwamba aoneshe ushirikiano, kwani mgeni yule anatoka makao makuu, atawasaidia.
Mzee anasema wao siyo wezi, bali walikamatwa na wanajeshi wakiwa wanaelekea hospitali, kijana aliyekamatwa naye ni mtoto wa dada yake na ana kidonda kisichopona.
Kijana anaonesha kidonda chake ambacho hakipo kwenye hali nzuri.
Wanapishana na wanawake waliotoka kuchota maji, msimuliaji anamwambia hao ni wafungwa wa zamani.
Msimuliaji anamwambia mgeni huenda wafungwa wale wanasema ukweli. Mgeni anamwambia atawahoji baadaye ili ajue.
Msimuliaji anamwambia atasaidia kwenye kutafsiri, Joll anamwambia hataweza, kuna mchakato mrefu, utamchosha.
Joll anaenda kuwahoji wafungwa, vinasikika vilio vya mateso makubwa.
Baadaye Msimuliaji anamuuliza vipi kama wafungwa hao wameshasema ukweli na hawana cha kusema tena? Anajuaje kama mtu amesema ukweli?
Joll anamjibu kuna sauti fulani mtu huwa anaitoa anaposema ukweli, mafunzo na uzoefu walionao huwa wanaijua sauti hiyo.
Msimuliaji anamuuliza kama anaweza kujua mtu anasema ukweli kwenye mazungumzo ya kawaida.
Joll anamjibu huwa wanaweza kwenye hali fulani, mfano mahojiano, mtu anaanza kusema uongo, wanampa mateso, anasema uongo tena, wanampa mateso, kadiri mateso yanaendelea, inafika mahali mtu anaanza kusema ukweli na hapo ndipo wanaijua sauti ya ukweli.
Msimuliaji anajiambia alichoondoka nacho kwenye maelezo ya Joll ni kwamba maumivu ndiyo ukweli, huwezi kujua ukweli bila maumivu.

Msimuliaji ni hakimu, baada ya Kanali Joll kuondoka anapokea ripoti fupi inayosema wakati wa mahojiano, mfungwa alijaribu kumshambulia afisa aliyekuwa anamhoji, katika kujihami afisa akamsukuma na kuanguka chini, juhudi za kumuokoa hazikufanikiwa.
Msimuliaji anamuita mlinzi aliyekuwepo wakati hilo linatokea na kumwambia aandike maelezo.
Anaeleza mfungwa alitaka kumshambulia afisa, akaitwa kusaidia, alipofika akakuta mfungwa tayari ameanguka chini.
Msimuliaji anamuuliza mlinzi iwapo afisa huyo alimwambia cha kusema, anajibu ndiyo. Anamuuliza tena kama alipofika alikuta mfungwa akiwa na pingu, anajibu ndiyo, halafu hapana.
Msimuliaji anaenda kwenye chumba cha wafungwa, anakuta mwili wa mfungwa mzee umefungwa na kuwekwa pembeni, huku mfungwa kijana akiwa amekaa kwenye kona.
Anaukagua mwili wa mfungwa aliyekufa na kukuta una majeraha kila mahali.
Anamwambia mfungwa kijana amwambie afisa anayemhoji ukweli na hataumizwa, aseme kila anachojua kwa ukweli na hilo pekee ndiyo litamsaidia.
Msimuliaji anamuonea huruma kijana yule, anamwambia mlinzi asimkaze mikono yake sana anapomfunga, asiache maiti ikae humo ndani na ampatie kijana chakula.
Msimuliaji anajiambia hakutaka kujiingiza kwenye hilo, kwani kazi yake ni hakimu, majukumu yake ni ya kiutawala, usimamizi na kusikiliza kesi na ameridhika na maisha yake na kazi, anachotaka ni kutekeleza majukumu yake mpaka astaafu.
Lakini tangu mwaka uliopita kumekuwa na ongezeko la uhalifu kwenye eneo hilo la mpakani, wizi, utekaji, uvamizi na mauaji vimeongezeka. Inaonekana maadui kutoka makabila jirani ndiyo wanafanya hayo.
Utawala unasema una taarifa kwamba maadui hao wanajipanga kwa uvamizi mkubwa wa kivita, hivyo wanapaswa kujipanga pia.
Msimuliaji anajiambia haoni jipya kwenye hali hiyo, kila mara tetesi huwa zinavuma maadui wanajiandaa kwa vita, lakini vita haijawahi kutokea. Matukio ya uhalifu huwa yanatokea mara kwa mara, lakini tishio la vita imekuwa ni hofu tu inayojengeka kwa watu.
Tangu kusambaa kwa tetesi hizo, ulinzi umeimarishwa maeneo ya mpakani na maafisa kutoka makao makuu ya ufalme wamekuwa wakitembelea maeneo hayo ya mipakani.
Msimuliaji anajiambia kipindi rahisi cha kazi yake kinaondoka na sasa ni kipindi kigumu kinachokuja.
Hakimu anaenda tena kumwangalia mfungwa kijana, anakuta ameumizwa kwa mateso aliyokuwa anapewa wakati wa mahojiano.
Anamuuliza iwapo aliyokiri kwamba kabila lao wanajiandaa kuvamia ufalme kivita ni kweli na kama anajua madhara ya kukiri kwake. Anamweleza jinsi ambavyo ufalme utavamia kabila lake na kuua watu wengi, ikiwepo wazazi na ndugu zake.
Kijana hamjibu chochote.
Analetwa daktari kutibu majeraha ya kijana, Kanali Joll anamsubiri apone amuongoze kwenda kwenye kijiji chao, anataka kwenda kufanya mashambulizi.
Hakimu anamwambia hilo halitakuwa sahihi, Kanali huyo hana uzoefu eneo hilo na anamtegemea kijana anayemhofia ndiyo amuongoze, haitaleta matokeo mazuri.
Anamwambia kwa maoni yake anashauri asifanye uvamizi huo, maana makabila hayo wana uzoefu mkubwa wa eneo hilo kuliko yeye hivyo kabla hata hajawafikia watakuwa wameshaondoka.
Kanali anamjibu ana wajibu wa kutekeleza, hivyo atautekeleza na kisha kutathmini matokeo baada ya kutekeleza, siyo kabla.
Hakimu anaendelea kumtahadharisha kwamba vitu vingi anavyotegemea siyo sahihi, ramani walizonazo zimechorwa kwa maelezo ya watu, hakuna ambaye amewahi kufika na kujionea.
Maandalizi yanakamilika na Kanali na wanajeshi wake wanaondoka wakiongozwa na mfungwa kijana.
Hakimu anawasindikiza mpaka njia inapoishia, anamtakia kanali heri na kurudi. Anajiona amepunguza mzigo mkubwa kwa kubaki mwenyewe.
Msimuliaji anapata ndoto anatembelea eneo lenye makazi ya zamani yaliyofukiwa na mchanga.
Anaona jinsi hayo yalikuwa makazi ya watu, ambao walijiona ni muhimu na kutekeleza majukumu yao ila sasa hawapo tena.

Ndoto hiyo imekuwa inamrudia mara kwa mara.
Siku nne baada ya Kanali kuondoka wanajeshi wanakuja na kundi la wafungwa wa kivita.
Hakimu anawasogelea na kugundua wale ni kabila la wavuvi na siyo kabila la wafugaji ambao ndiyo maadui wa ufalme.
Anawauliza wanajeshi wale kwa hasira kwa nini wamekamata watu hao, wanamjibu kanali amewapa maelekezo hayo.
Anawaambia hao hawana msaada wowote kwa kuwa hawahusiki kabisa na uvamizi.
Wanamwambia wakati wanapita, watu hao walijificha, kanali aliposema wakamatwe, hawakuweza kuwahoji kwa sababu lugha yao ni tofauti, hivyo akaagiza waletwe kambini.
Hakimu anasema huo ni upotevu wa rasilimali, anazidi kumdharau kanali na kuona hajui anachofanya.
Anaagiza wafungwa hao waweke ndani ya uzio na wapatiwe chakula.
Kwa siku chache wafungwa wale wameshayazoea maisha na kuyafurahia, wanapata chakula kila siku kitu kinachoonekana kuwaridhisha.
Tetesi zinazuka kwamba wafungwa hao wana ugonjwa wa mlipuko ambao utasambaa kwa watu wengine, hilo linapelelea wafungiwe kwenye uzio na kurushiwa chakula kama wanyama.
Mtoto wa mmoja wa wafungwa hao anaumwa na kufa.
Hakimu anaandika barua kwa hasira kwenda makao makuu, wakitaka atumwe mtu mwenye uzoefu na mpaka huo, maana kinachofanyika sasa siyo sahihi.
Anaichana barua ile, anafikiria jinsi Kanali Joll amekuja kumletea matatizo ambayo hayakuwa na umuhimu.
Kanali na wanajeshi wanarejea usiku, wamebeba wafungwa wengi zaidi wa kivita, watu wanashangilia kurudi kwao. Hakimu anaangalia kwa mbali na kurudi kulala.
Kesho yake Kanali analala siku nzima, Hakimu anaenda kwenye shughuli zake za kiutawala, hajisumbui kuangalia wafungwa walioletwa.
Hakimu anakutana luteni aliyeambatana na kanali kwenye uvamizi, anawapongeza kwa kurudi salama. Anamuuliza kwa nini hakumwambia wavuvi waliowakamata kama wafungwa hawana msaada? Luteni anamjibu alijaribu kumwambia, lakini kanali akamjibu wafungwa ni wafungwa, hakutaka kuendelea kubishana naye.
Kanali anaanza mahojiano na wafungwa, mwanzo hakimu alimuona ni afisa mvivu tu. Lakini kwenye kusaka ukweli, hakuwa na uvivu wowote. Alianza mahojiano alfajiri na kwenda mpaka usiku wa manane.
Kwa kipindi chote hakimu alikuwa anamkwepa kwa kujipa majukumu yanayomuweka mbali.
Hakimu anamuita binti ambaye huwa ana mahusiano naye na kulala naye. Anapoamka asubuhi anakuta amelala chini, anamuuliza kulikoni anamjibu alimfukuza kitandani akiwa usingizini.
Siku moja hakimu anatembelewa na kanali ofisini kwake, anampa taarifa kwamba jukumu lake kwa sasa limeisha, anarudi makao makuu akaandae ripoti.
Hakimu anamuuliza kama mahojiano yake na wafungwa waliokamatwa yamekuwa na mafanikio, kanali anamjibu ndiyo yamekuwa na mafanikio, wamepata taarifa za kutosha.
Hakimu anamuuliza nini hitimisho lake, je wapo salama na wasiwe na hofu? Hamjibu, anainuka na kuondoka.
Siku inayofuata mapema alfajiri kanali anaondoka. Hakimu anaenda walipo wafungwa na kuagiza waondolewe na eneo lisafishwe.
Anaona wafungwa wakitolewa, ambao wanaonekana kuchoka kuliko walivyokuwa siku tano zilizopita alipowaona.
Hakimu anatamani hayo yaliyotokea yasingekuwa yametokea, anatamani ufalme ungetawaliwa kwa sheria na haki.
Anaagiza wafungwa wahudumiwe vizuri na kurudishwa kwenye maisha yao.

👉2
Hakimu anakuta mwanamke ombaomba njiani, anarudi na kukuta bado yuko pale ni wa kabila la wafugaji.

Anaweka sarafu kwenye chomo chake cha kuombea na kumwambia hapaswi kuwa hapo muda huo.
Siku inayofuata hakumuona, anawauliza walinzi wanamwambia ni kipofu, alikuwa mmoja wa wafungwa, ameachwa baada ya wenzake kuondoka.
Siku chache baadaye anamuona tena akipita njiani, anaagiza aletwe kwake, anamuuliza kwa nini anaomba na anakaa wapi. Anajibu hana pa kukaa. Hakimu anamuuliza anaweza kufanya kazi gani, anajibu usafi.
Hakimu anamwambia haruhusu watu kuwa omba omba, hivyo atampa kazi ya usafi na atalala na mfanyakazi mwingine.
Mwanamke yule anamjibu yeye si mtu sahihi kwa kazi hiyo, hakimu anamwambia asijali kwa upofu alionao.
Siku inayofuata Hakimu anamkuta yule mwanamke kipofu akiwa nje peke yake, miguu inamuuma hawezi kutembea. Anamsaidia kuingia ndani, anaona vidonda vyake haviko vizuri, anachukua maji na kuvisafisha na kuahidi kumfunga kwa bandeji nzuri, zoezi hilo linamchosha na anapumzika, usingizi unampitia, anaamka na kukuta mwanamke yule hayupo.
Siku inayofuata anampa chakula na kuzungumza naye wakati anakula, anamwona akiwa anaangalia kwa upande. Mwanamke huyo anamwambia akiangalia mbele anaona ukungu, ila akiangalia kwa pembeni anaona kidogo, hiyo ndiyo inamsaidia kutembea na kufanya mambo mengine.
Mwanamke anamweleza hakuwa na tatizo hilo awali, bali limejitokeza baada ya kupigwa na kuteswa.
Usiku zoezi la kusafisha vidonda vyake linaendelea, Hakimu anafanya kazi hiyo mpaka anasinzia, anakuja kustuka mwanamke naye ameainzia na wa baridi, anamfunika.
Zoezi la kusafisha vidonda linakuwa la kumuogesha pia, hakimu huyo anamvua nguo, kumuogesha na kumpaka mafuta mwili mzima.
Ni zaidi ya wiki sasa yuko na mwanamke huyo, anamlisha, kumsafisha na kumpa pa kulala kila siku.
Kwa kuwa anajua haoni vizuri, amekuwa hajali, anavua nguo hata mbele yake, akijua hamuoni.
Tetesi zinaanza kusambaa kwamba hakimu anatembea na yule mwanamke kipofu.
Mwanamke yule anaungana na wafanyakazi wengine wa pale na wanashirikiana vizuri.
Hakimu anamwuliza kama anaipenda kazi anayofanya, anamjibu ni bora kuliko kuomba.
Anamwambia kama atataka kuondoka anaweza kuagizwa arudishwe kwa wenzake, anamjibu hana pa kwenda.
Mchana mwanamke yule anafanya shughuli zake, usiku anaenda chumbani kwa hakimu.
Lakini hakimu hajawahi kumtamani kimapenzi, wala kufanya naye kimapenzi. Mwanamke huyo anaonekana bado ni binti, huku hakimu akiwa mtu wa makamo.
Usiku mmoja tamaa inamuingia hakimu na anafanya mapenzi na mwanamke yule.
Hakimu anawahoji walinzi wote waliokuwepo wakati wafungwa wanahojiwa.
Wote wanamjibu hawakuruhusiwa kuingia wakati wa mahojiano.
Anawabana wawili ambao walikuwa zamu siku ambayo mmoja wa wafungwa alikufa. Mfungwa aliyekufa ni baba wa mwanamke anayekaa naye. Wanamjibu baba huyo alihojiwa kwa muda mrefu kuliko wengine, baadaye akatoka ameumia sana, akagoma kula na kufa.
Anawauliza kuhusu upofu wa yule mwanamke, wanamjibu hawajui aliupataje, maana walikuwa wanasimamia wafungwa wengi.
Majira ya baridi yamefika, shughuli zimepungua na hata wanajeshi wamepungua kambini.
Kipindi cha baridi kama hicho watu wa kabila la wafugaji huja na kupiga kambo nje ya mji huo na kufanya biashara ya kubadilishana vitu.
Hakimu amekuwa anadhibiti sana biashara hiyo isihusishe fedha wala pombe, kwa sababu hakutaka izalishe walevi na ombaomba.
Lakini msimu wa baridi wa mwaka huu watu hao hawajaja. Kuna mvutano mkubwa unaoendelea na vita inategemewa muda wowote.
Hakiku amekuwa akiishi na mwanamke yule kama mpenzi. Mara nyingi wanapoongea naye anajifunza jinsi malezi ya kabila lao yalivyo ya kufuata misingi fulani na kuwa na msimamo.
Mfano binti amekuwa anamwambia kama mtu anataka kufanya kitu anapaswa kufanya, kama hataki asifanye.

Hakimu anamuuliza kama kuishi naye ametaka, binti anamjibu anafanya hivyo kwa sababu hana pa kwenda.
Mwanamke anamlalamikia hakimu kwamba anaongea sana na kila mara anahoji maswali.
Anamjibu kwamba wakati wa mahojiano wakikuwa wanaweka uma kwenye moto mpaka unakuwa mwekundu, kisha wanachoma nao watu.
Kwake walimwambia watamchoma macho, ila hawakufanya hivyo, badala yake waliyafungua macho yake na kuweka uma wa moto mbele yake, tangu hapo ndiyo amekuwa haoni vizuri.
Ila anasema kwa sasa anaendelea vizuri, uoni wake umeanza kurudi.
Hakimu anamuuliza anawachukuliaje wale waliomfanyia hayo, analala na kumjibu amechoka kuongea.
Hakimu anamuacha mwanamke yule na kwenda kwenye chumba kingine alipo mpenzi wake wa zamani. Anaingia na anampokea kwa shauku kubwa, wanafanya mapenzi, anaona jinsi mwanamke huyo anavyomvutia.
Anarudi kwenye chumba chake, mwanamke yule bado amelala, hana hisia zozote za kimapenzi kwake, lakini hajui kwa nini anaendelea kuwa naye.
Baada ya kufikiria sana hilo anaona mateso ambayo mwanamke yule amepitia ndiyo yanamfanya hakimu amuonee huruma na kumpa nafasi. Ila anaona hilo ni kujiadhibu yeye kwa kosa la kabali.
Hakimu anamtembelea mpenzi wake wa zamani mara kwa mara na kufanya naye mapenzi.
Anakumbuka tangu ameanza kazi kwenye mpaka huo, miaka mingi imepita, amekuwa na mahusiano na wanawake wengi. Kuna wakati anaona ndani yake kuna nafsi mbili, nafsi yake halisi na nafsi ya mapenzi. Anaona kama nafsi ya mapenzi imekuwa na nguvu na kumtawala maisha yake yote.
Ila anaona nguvu hiyo ikipungua kadiri umri unavyokwenda. Zamani alivutiwa kimapenzi na mwanamke yeyote, ila sasa ni wanawake wadogo na warembo tu ndiyo wanamvutia kimapenzi.
Anapatwa hasira kila akijiuliza nini kilimfanya amlete mwanamke huyo kwenye maisha yake.
Kila akimwangalia haoni cha kumvutia kwake. Anajaribu kukumbuka labda alimuona wakati analetwa kabla hajaumizwa, lakini hapati kumbukumbu zake.
Usiku mwabamke yule anamwamsha, anamwambia anagomba akiwa usingizini, hakimu hana kumbukumbu kama hata alikuwa anaota.
Hakimu anajaribu kumuuliza maswali ya siku waliyokuja ili aweze kupata picha yake, lakini hapati picha.
Kundi la wanajeshi wapya wanakuja kwenye mpaka ule, kuchukua nafasi ya wanaoondoka.
Kundi hilo linaongozwa na afisa ambaye ni kijana, ambaye atakuwa mmoja wa wafanyakazi.
Wanafanya maongezi na hakimu, anaeleza jinsi safari ya kufika hapo ilivyokuwa ngumu, njiani amepoteza wanajeshi wapya watatu, ambao walitoroka njiani. Afisa hiyo anawaita ni wasumbufu na haoneshi kusikitika kuwapoteza.
Hakimu anamuuliza kama anajua sababu iliyowafanya watoroke, anajibu hajui, kwani wamekuwa wanahudumiwa vizuri.
Wanaongea kwa muda mrefu, hakimu anapenda nguvu alizonazo na mtazamo wake kuhusu eneo hilo la mpaka.
Afisa anamwambia makao makuu kuna tetesi kwamba kutakuwa na vita ya kuwafukuza watu wa mabila la wafugaji kurudi milimani.
Hakimu anamwambia watu hao huwa wana maisha ya kuhamahama, siyo rahisi kuwaweka eneo moja, hawatakubali kufukuziwa kwenye milima.
Afisa yule anamjibu hiyo ndiyo maana ya vita, kumlazimisha adui afanye asichokuwa tayari kufanya.
Afisa anamuuliza hakimu kwa uzoefu wake pale kwa miaka mingi, kabila hilo la wafugaji wanataka nini hasa?
Hakimu anamjibu amekuwa anafanya kazi hapo kwa miaka zaidi ya 20 na kitu kimoja wafugaji hao wanataka ni wao waondoke. Anaeleza kwamba miaka 100 iliyopita ufalme ulivamia na kuchukua eneo lao na kujenga makazi hayo. Eneo lililochukuliwa ni lenye rutuba, pembeni ya ziwa na hivyo kwa sasa wanasumbuka kulisha mifugo yao.
Anaeleza wafugaji hao hawajakata tamaa, wanaamini siku moja wataondoka na wabaki huru na eneo

lao.
Na sasa wana matumaini makubwa na hilo kwa sababu ziwa limeanza kukauka, hivyo wanajua miaka siyo mingi maisha hapo hayatawezekana bila maji, hivyo wavamizi wataondoka na wao wafigaji kubaki huru.
Afisa yule anamjibu hilo halitatokea, hata kama maji yatakauka, ufalme hauwezi kuachilia eneo hilo, maana ni mpaka muhimu kiulinzi kwenye ufalme.
Hakimu anaona jinsi afisa yule atalavyokuwa amemchukulia yuko upande wa wafugaji. Lakini hajali, anachotaka ni kumalizia miaka yake michache ya utumishi iliyobaki kwa amani.
Ndoto ya mji uliofukiwa inamrudia tena, safari hii anaona binti akijaribu kujenga mji huo upya, lakini hauna uhai. Anamsogelea binti kwenye ndoto na kugundua ni mwanamke anayelala naye.
Anastuka na kumkuta amelala usingizi.
Hakimu anamuuliza mwanamke yule kuhusu maisha yake kabla hajaanza kukaa naye, anamweleza mengi, ikiwa ni pamoja na wanajeshi waliokuwa wanamwingilia kimapenzi wakati ameumizwa.
Hilo linampa hasira hakimu, kila anapowaona wanajeshi wakiwa kwenye paredi, anajiambia baadhi hapo walishatembea na mwanamke yule.
Taarifa zinakuja kwamba baadhi ya wanajeshi wapya waliotorokea njiani wamekufa kwenye hali mbaya ya hewa wakati huo wa majira ya baridi.
Hakimu anamshawishi luteni maiti hizo zikachukuliwe na kuzikwa kwa heshima, luteni alikuwa anaona hawezi kuhangaika na maiti hizo kwenye hali hiyo mbaya ya hewa. Hakimu anamwambia kwa kuwapa maziko ya heshima, itaongeza morali kwa wanajeshi wake, luteni anakubali.
Hakimu anajiambia ni jambo linalomshangaza, mtu asafiri umbali mrefu, akaribie kufika halafu aamue kuachana na safari hiyo, kwenye mazingira ambayo ni hatari kwake.
Wakiwa wamelala, mwanamke yule kipofu anamtomasa hakimu ili wafanye mapenzi. Hakimu anaondoa mkono wake na kumwambia siku nyingine. Mwanamke anamwambia anajua huwa ana wapenzi wengine, je huwa anawafanyia hivyo pia?
Hakimu hakumjibu, lakini tangu siku hiyo hakulala naye kitanda kimoja tena. Mwanamke hakuwa na malalamiko yoyote kwake.
Hakimu anashindwa kumuelewa, anajiuliza ndiyo makuzi yao ya kutokujali au kwa kuwa hana pa kwenda. Anaona jinsi utulivu wa mwanamke yule unavyomshinda yeye binafsi.

👉3
Hakimu anajiambia kabla hajaondoka kuna nyaraka mbili anapaswa kuziandika. Ya kwanza ni kuhusu kujenga upya mahusiano mazuri na kabila la wafugaji. Ya pili hajui hata inahusu nini.
Kwa siku mbili anakazana kufikiria aandike nini, lakini hapati cha kuandika. Anaamua kuihifadhi karatasi hiyo na kuanza safari.
Anachukua wanajeshi wapya wawili, mzee mzoefu pamoja na mwanamke ambaye amekuwa anakaa naye. Anamwambia anamrudisha kwao au karibu na kwao.
Wanaianza safari, ni ndefu, ya wiki mbili, wamebeba mahitaji yote muhimu. Safari ni ta kulizunguka jua, kisha kuvuka jangwa na kuelekea maeneo ya kabila hilo la wafugaji.
Safari inakuwa ngumu na inayowatesa, wanaishiwa maji na kulazimika kutumia maji ya chumvi kitu kinachopelekea waharishe sana.
Lakini mwanamke yule haonekani kusumbuliwa na safari, anaonekana kuwa mzoefu kwa safari za aina hiyo.
Hakimu analala na yule mwanamke kwenye hema moja, kwa siku za mwanzo bado hana hisia naye kama ilivyokuwa awali. Lakini usiku wa saba, mwanamke yule anamtomasa kimapenzi, anapatwa na hisia na wanafanya mapenzi.
Baada ya kufanya mapenzi hakimu anajaribu kutafakari kama hisia alizopata hapo ni za kweli au kwa kuwa anajua siku siyo nyingi hawataonana tena.
Bado anashindwa kuzielewa hisia zake kwa mwanamke huyo.
Safari bado ni ndefu, Hakimu anamuuliza muongozaji zimebaki siku ngapi wafike kwenye milima, anamwambia mbili mpaka tatu, hana uhakika kwa sababu hajawahi kupita njia hiyo.

Wanapigwa na dhoruba kali, upepo mkali wa kimbung'a unawajia, wanapoteza hema moja na vitu vingine.
Baada ya dhoruba wanalazimika kupunguza baadhi ya mizigo ili waweze kwenda haraka na kwa kuwa farasi walionao nao wamechoka.
Siku ya kumi wanaona watu wakiwa mbele yao, wanaongeza mwendo ili wawafikie ila nao wanaongeza mwendo pia. Wakipunguza mwendo nao wanapunguza. Hakimu anawaambia wenzake haina haja ya kupoteza nguvu kukimbizana na watu hao, waendelee na safari yao.
Kwa siku 12 wako njiani, wamechoka sana, ukaribu wake na mwanamke yule umekuwa mkubwa kwa siku hizo kuliko miaka yote ambayo amekaa naye.
Wanakaribia watu ambao ni kabila la wafugaji, watu hao wanawaelekezea silaha, hakimu anaonesha ishara kwamba hawajaja kwa shari.
Anamwambia mwanamke yule kwamba anaweza kwenda kwa watu wale, awaeleze lengo la safari ya hakimu na kisha achague kama atabaki nao wampeleke kwa ndugu zake au atarudi na hakimu.
Mwanamke anamjibu hayuko tayari kurudi naye, hilo linamuumiza sana hakimu.
Mwanamke anakuwa njia ya kupena ujumbe kati ya hakimu na wafugaji wale, mwisho wanataka apewe farasi na vitu vya kumsaidia, anapewa vitu hivyo kisha wanaagana, hatua hiyo inamuumiza hakimu kwa kuwa hatamuona tena mwanamke huyo.
Safari ya kurudi inaanza, mwanzo inaoneokana rahisi na wote wana nguvu ya kwenda haraka.
Lakini siku ya pili mwanajeshi mmoja anaumia mguu na inabidi abebwe na farasi.
Safari inakuwa taratibu zaidi, pamoja na mwanajeshi kuumia, lakini pia kwa kuwa yule mwanamke hayupo tena, watu hawana msukumo kama mwanzo.
Wanakazana na safari na mwisho wanakaribia mji wao, wanakuja kupokelewa na farasi lakini watu wanaowapokea hawawajui.
Wanapofika wanagundua jeshi zima liko pale, vita dhidi ya wafugaji inakaribia kuanza.

👉4
Hakimu anapelekwa mpaka kwenye ofisi yake, anakuta kuna mtu amekaa kwenye meza yake na anakagua mafaili.
Anamuuliza kama kuna anachoweza kumsaidia, mtu huyo anamuuliza alikuwa wapi.
Hakimu anajibu alikuwa na safari nje ya mji kwa mambo yake binafsi.
Mtu huyo anamwambia wametumwa kutoka makao makuu ya ufalme, hakimu huyo amekuwa anashirikiana na maadui.
Hakimu anamwambia hapo hakuna adui, bali kuna makabila ya wafugaji yanayowazunguka.
Mtu yule hamjibu tena, hakimu anapelekwa kwenye chumba kinachotumika kama gereza.
Anafungwa huko, anapewa chakula mara mbili kwa siku na kila baada ya siku moja anatolewa nje kujisafisha na kufanya mazoezi.
Akiwa kwenye chumba hicho anapata picha watu waliopitia mateso wakiwa hapo. Anamkumbuka mwanamke aliyekuwa anaishi naye, ambaye baba yake aliteswa mpaka kufa kwenye chumba hicho huku na yeye pia akiteswa mpaka upofu.
Hakimu anaona wakati wa yeye kuteswa pia umefika na hana yayote wa kumtetea au kuwa upande wake.
Lakini anajikna yuko huru, hayuko tena chini ya amri ya kutekeleza kile anachopangiwa na ufalme ambacho anaona siyo sahihi. Uhuru huu ndiyo unaompa hali ya kuridhika kuliko kitu kingine chochote.
Ndoto ya mji uliofukiwa inaendelea kumjia kila mara, japo anashindwa kupata tafsiri yake.
Hakimu anapelekwa ilipokuwa ofisi yake, anakuta imebadilika sana, imesafishwa na kupangiliwa vizuri.
Anayeitumia ofisi kwa sasa anamwambia atamsomea mashtaka yanayomkabili ili ajie ukubwa wa hali yake.
Anamsomea mashtaka kama ifuatavyo;
1. Uwajibikaji wake kwenye kazi umekuwa siyo wa kuridhisha.
2. Kuna ubadhulifu wa fedha za ofisi.

3. Amekuwa anajihusisha kimapenzi na wanawake wa mtaani, wanawake ambao wanajeshi pia wanajihusisha nao kimapenzi, hivyo ameidhalilisha ofisi yake.
4. Aliandaa safari ya kwenda kutoa siri za uvamizi kwa kabila la wafugaji hivyo amekuwa msaliti.
Hakimu anasikiliza na kusema atajitetea mahakamani.
Hakimu anamwangalia mtu yule na kuona ni kijana anayejaribu kutekeleza wajibu wake akitegemea kupanda cheo kupitia kuwaumiza wengine.
Anarudishwa kwenye chumba cha gereza, hajapigwa, kuteswa wala kunyimwa chakula. Ila hajapata nguo za kubadilisha tangu awe huko.
Anajiambia hatakubali hali hiyo imdhalilishe au ajidharau.
Anamkumbuka yule mwanamke na kujiona sasa yuko kwenye viatu alivyokuwa anapitia kwa wakati anamchukua.
Amakuwa anasikia mazungumzo ya kinachoendelea, japo hakuna anayemwambia nini kinaendelea.
Alisikia wanajeshi waliondoka kwenda kuwashambulia wafugaji, lakini siku chache baadaye wamerudi kimya kimya, hakuna kelele za ushindi na wala hakuna wafungwa wa kivita. Hakimu anafurahia hilo.
Siku moja hakimu amechelewa kuletewa chai, ana njaa, anagonga mlango kwa nguvu, mlinzi anamfungulia na kumuuliza anataka nini.
Anamwambia anataka chai, pia hiyo ni siku yake ya kujifanyia usafi, anamuomba ampeleke jikoni akapate maji ya moto.
Mlinzi anampeleka, akiwa anachota maji anaangalia zinapokaa funguo, anachukua ufunguo ambao anajua unaingiliana na milango mingi.
Usiku anatumia ufunguo huo kutoroka, anaumia wakati anatoroka lakini anajisukuma licha ya kuwa na maumivu makali.
Anajificha kwenye moja ya vyumba vya wasichana aliokuwa anatembea nao. Anaingia kwenye uvungu wa kitanda.
Anasikia msako ukipita chumba kwa chumba, mlango wa chumba alipo unafunguliwa, mtu anaingia na kuangalia kisha anatoka.
Anaona ameshinda mtihani wa kwanza. Anasubiri mchana wa jua kali, muda ambao watu wanakuwa wamepumzika na anatoka.
Mlinzi mmoja anamsimamisha, inaonekana hamjui, anamdanganya alikuwa anaumwa na amekuwa ndani kwa muda, hajui kinachoendelea.
Mlinzi anamwambia wafugaji wameharibu mazao yao na wanajeshi wachache wamerudishwa baada ya kuumwa kutokana na maji na hali mbaya ya hewa.
Hakimu anapata picha ya kinachoendelea, anamuacha mlinzi yule na kuondoka.
Anafikiria jinsi mpango wake wa kutoroka unavyoweza usizae matunda, ataweza kwenda mpaka wapi? Anafikiria jinsi wakimkamata tena watakavyomtesa kama msaliti, hasa watakaposhindwa vita na wafugaji.
Lakini anajiambia watamuua kwa vyovyote vile, hivyo hatawarahisishia kazi hiyo kwa kufia kwenye mazingira magumu.
Anaamua arudi kwenye gereza, ambapo atapata chakula na maji mpaka pale watakapokuja kumuua.
Anaporudi mlinzi anampokea kwa ukali na kumwambia asije akasema alitoroka, atahatarisha kazi yake.
Hakimu anamwambia ajiulize kwa nini ametoroka, kama kweli alikuwa anashirikiana na wafugaji si angeenda kwao? Anamwambia hatasema chochote, yeye atunge uongo wake atakavyo, anachotaka yeye ni chakula na maji.
Anapewa chakula na maji na kuendelea kusubiri.
Usiku akiwaa kwenye gereza, Hakimu anasikia sauti za kushangilia, anashawika kutoka kwenda kuangalia. Anaenda na kuona ni wanajeshi wamerudi, wakiwa na wafungwa 12 ambao wamewafunga kwa kupitisha nyaya kwenye nyama zao.
Watu wamekusanyika kuangalia, wafungwa wanawekwa katikati na kanali Joll anatoa maelekezo wapigwe.
Hakimu anatamani arudi kwenye gereza ili asishuhudie mateso wanayopata wafungwa hao, ila

anashindwa kuondoka.
Wafungwa wanapigwa sana, wanalia kwa uchungu. Baadaye anamuona kanali akichukua nyundo kubwa na kumpa mwanajeshi awapige nayo wafungwa.
Hakimu anashindwa kujizuia, anasema kwa sauti hapana, siyo sahihi kufanya hivyo, hata kama ni wafungwa wa kivita, siyo haki kuwatesa hivyo
Kabla hakamaliza kuongea anasikia kishindo kikubwa na maumivu, anapigwa sana na wanajeshi wake kisha kurudishwa kwenye gereza akiwa kwenye maumivu makali.
Hakimu anapelekwa kwenye iliyokuwa ofisi yake, anamkuta kanali Joll amekaa na kopo lenye mabaki ambayo hakimu alikuwa amekusanya.
Joll anamwambia katika kukagua vitu vyake, wamekuta jumbe hizo ambazo zimeandikwa kwa alama za siri, hivyo wanamtaka aeleze maana zake.
Hakimu hajui, yeye alikuwa anakusanya tu. Anatumia nafasi hiyo kueleza maana ya jumbe hizo ni mawasiliano ya wafugaji kuhusu mateso ambayo Joll aliwapa wafungwa waliokuwepo mpaka wakafa.
Joll anamwambia hakimu anachofanya hakimsaidii, atahukumiwa siku siyo nyingi.
Hakimu anamwambia mbona hawampeleki kwenye kesi yake ya kujibu? Anajiambia anaweza kuwakabili vizuri kisheria, japo watatumia nguvu kumshitaki.
Anajiambia wanajua kwa sasa ana nguvu na akili ndiyo maana hawamshitaki, wanataka kumfungia gerezani kwa muda, achoke na kupoteza akili ili wanapomshitaki asiweze kujitetea.
Kanali Joll anamwambia hakimu siyo kwamba wanamuogopa, kwani hakuna aliye upande wake. Watu wote walikuwa wamemchoka kwa tabia zake mbovu, hasa ya umalaya. Hakimu anamjibu maisha yake binafsi hayawahusu.
Kanali anamwambia hakimu kwamba alipokuja, mpango wake ilikuwa ni kumtoa kwenye madaraka na kumwacha awe huru kuendelea na umalaya wake. Ila sasa anaona hakimu anataka kuonekana yeye ndiye mtu pekee aliye sahihi na anayesimamia haki, aliye tayari kufa kusimamia misingi yake.
Joll anamwambia asijidanganye, atakufa na hakuna atakayemkumbuka kama shujaa, kwani hata wananchi kwa sasa wanamchukulia kama msaliti kwa kuungana na maadui.
Hakimu anamwambia wafugaji wale siyo maadui, bali adui mkubwa ni yeye kanali na ufalme kwa kile wanachofanya.
Joll anamwambia hakimu atoe maelezo ya mazungumzo aliyofanya na wafugaji alipowatembelea.
Hakimu anakataa kutoa maelezo yoyote.
Joll anawagiza maafisa wamshughulikie, anaenda kupewa mateso makali.
Hakimu anaamua hakuna kiwango cha mateso kitakachomvunja afanye wanavyotaka wao.
Anateswa mno, kwa siku mbili hajapewa chakula wala maji, lakini bado anabaki na msimamo wake.
Anapigwa kila siku, ana vidonda ambavyo havisafishwi, mwili wake ni mchafu na unanuka, hapewi hata nafasi ya kujisafisha.
Wanamdhalilisha kila siku kwa kumtoa nje na kumpiga akiwa uchi, lakini bado hakimu amebaki na msimamo wake.
Wanamchukua na kumpeleka kwenye mti, wanamning'iniza kwa kutumia kamba. Hakimu anauliza Joll yuko wapi, anaambiwa kama kuna kitu anataka kusema aseme hapo.
Hakimu anasema alipoenda kwa wafugaji hakuzungumza nao chochote kuhush vita, alikuwa amemrudisha mwanamke aliyekuwa anaishi naye, yalikuwa mambo binafsi tu.
Wanamwambia bado haitoshi, hakimu anaendelea kusema anataka kuishi kama wengine wanavyoishi, uhai wake ni kitu anachothamini.
Wanavuta kamba wanayomning'iniza nayo, anapata maumivu makali. Watu wamemzunguka pamoja na watoto, wanafurahia mateso anayotapata.

👉5
Hofu ya uvamizi wa wafugaji inakuwa kubwa baina ya watu.
Inasemekana wanakuja usiku, wanachukua wanachotaka na kudhuru watu.
Hivyo watu wanatakiwa kuweka vitu vyote ndani usiku na kutokutembea usiku.

Maduka yanavamiwa na kuibiwa, inasemekana ni wafugaji.
Mabinti wanabakwa, inasemekana ni wafugaji.
Kinachowashangaza watu ni kwa nini wanajeshi hao washindwe kuwadhibiti wafugaji hao?
Hakimu amerudishwa kwenye chumba cha gereza, lakini hakijafungwa. Ni kama hakuna anayemhofia kwamba atatoroka, hali yake ni dhoofu.
Anasikia kila kinachoendelea, kundi kubwa la wanajeshi wameondoka, hawajarudi na hakuna taarifa zozote.
Tetesi ni nyingi, zipo taarifa kwamba wameshindwa, zipo nyingine kwamba wamewashinda adui.
Wanajeshi walioachwa kwenye mji nao hawadhitiki, wamekuwa wanafanya uhalifu mbalimbali kwa wananchi. Kanali Joll ameondoka na jeshi kwenda kwenye mapambano, afisa mwingine aliyeachwa kama kiongozi aitwaye Mendel haonekani kujali.
Mendel ndiye aliyekuwa anaongoza mateso ya hakimu.
Anamtembelea hakimu na kumwambia anapaswa afanye kazi kujipatia chakula, hawawezi kuendelea kumlisha.
Hakimu anamwambia sheria haisemi hivyo, yeye ni mahabusu, mahabusu hapaswi kufanya kazi, anatakiwa kulishwa.
Mendel anafungua mlango na kumwambia wewe siyo mahabusu, uko huru kabisa, ondoka ukajitegemee.
Hakimu anamwambia kabla hajaondoka alitaka kumuuliza swali moja, je huwa anawezaje kula chakula baada ya mateso anayokuwa amewapa watu siku nzima?
Mendel anampiga na kumwambia nenda kafie mbali.
Hakimu anazunguka mitaani kuomba chakula. Watu wanampokea kwa huruma, wanampa pole kwa yaliyomkuta.
Wengi wanamwambia wakati yeye akiwa kiongozi hakukuwa na shida, ila tangu wageni wamekuja maisha yamekuwa ni shida.
Anakubaliana nao, anaeleza jinsi yote hayo yamesababishwa na mambo binafsi na yasiyo na umuhimu.
Ana njaa kali, anaenda kwenye jiko la alipokuwa anaishi, anamkuta mpishi aliyemzoea kwa miaka mingi.
Mpishi anamwambia mabinti waliokuwa wanamsaidia wote wameondoka, watu wengi wanatoroka kuondoka.
Hakimu anamwambia kwa sasa anachotaka ni chakula tu, hakuna kingine anahangaika nacho.
Anamweleza hata mapenzi amekuwa hayafikirii kwa sasa kama chakula.
Anamweleza ataendelea kuzunguka kuomba chakula na akiona amekuwa mzigo kwao ataenda kwa wafugaji aombe kuwasaidia kazi wampe chakula.
Ni miezi mitatu tangu jeshi liondoke na halijarudi wala hakuna taarifa zozote.
Tetesi ni nyingi, watu wametaharuki na wanaokumbia mji.
Wanajeshi hawana tena udhibiti, wanavunja nyumba za watu na kuchukua vitu, wanazuia watu wasiondoke kwenje mji.
Hakimu anajiambia kwa hali yake hawezi kuondoka na wengine, kwani hali ya hewa siyo nzuri na mwili wake ni dhoofu.
Lakini pia anajiambia amekaa hapo miaka mingi, hakuna hatari ya wafugaji. Hata sasa, wafugaji hao wameenda kujificha mbali, wanasubiri jeshi lichoke na kuondoka, kisha watarejea kuendelea na maisha yao.
Hakimu anaelekea kwenye kambi ya wavuvi, anaona ni bora kujiunga nao kuliko kuwa omba omba.
Anatafakari jinsi watoto, ndege na samaki wanavyoishi wakiwa huru, bila hofu ya chochote.
Anajiuliza kwa nini watu wazima hawawezi kuishi hivyo, anapata majibu kwamba tawala ndiyo zinafanya watu waishi kwa hofu.
Huwa zinatengeneza hofu isiyo ya kweli ili kuwafanya wananchi wazitegenee tawala hizo. Mfano usiku utawala unaweza kuwaibia wananchi wake, halafu mchana unaonekana unawalinda.
Hata kwenye vita, huwa vinatumika kama njia ya utawala kujiimarisha kwa wale inaowatawala.

Hakimu anajikumbusha kipindi akifanya kazo, jinsi alipenda kusimamia sheria na haki. Aliamini binadamu ni hatari, yeyote anayekuwa juu ya sheria lazima alete madhara makubwa kwa wengine.
Mara nyingi alifikiria kuacha kazi hiyo na akaishi maisha yake, lakini alipofikiria wangapi watakosa haki, aliamua kuendelea nayo, mpaka yalipomfika yaliyomfika.
Mandel na wanajeshi waliosalia wanaondoka, baada ya kupora vitu kutoka kwa raia, wamechukua farasi wengi na chakula chote. Mji unaachwa wazi, baadhi wa wananchi wanabeba vitu vyao na kuwafuata wanajeshi hao nyuma.
Wanajeshi walioenda kwenye mapambano hawajarudi, wakati wanajeshi waliosalia wanaondoka, Mendel anawaambia wananchi wanaondoka kwa muda tu, watarudi mambo yakiwa vizuri.
Mji unaachwa ukiwa hauna kitu, hakimu ni mmoja wa wachache waliosalia.
Hakimu anaingia kwenye nyumba aliyokuwa anaishi na kukuta vitu vyake karibu vyote viko kama vilivyokuwa, isipokuwa vichacha vilivyoondolewa.
Anaingia kwenye chumba chake na kujilaza kitandani akitafakari kilichotokea na mwisho anaoendea.
Anajiambia kama hatari ya uvamizi wa wafugaji ipo kweli, basi huo ndiyo mwisho wao, kwani wakija sasa hakuna ulinzi wowote.
Anatafakari jinsi maisha yalivyo kama mchezo wa kujidanganya, jeshi limekuja hapo, limewajaza watu uongo na limeondoka baada ya kuharihu kila kitu.
Anatafakari jinsi jeshi lenye silaha kubwa na za kisasa limeshindwa na wafugaji wanaotumia mikuki, wasiojua kusoma wala kuandika.
Anajipumzisha kwenye kitanda chake akiwa tayari kwa lolote.

👉6
Hakimu anajaribu kuwakusanya wananchi waliobaki na kuangalia watazaje kuendesha maisha yao baada ya yaliyotokea.
Tatizo ni chakula hakuna na hali ya hewa siyo nzuri.
Wananchi wanamsikiliza kama kiongozi, japo bado hofu ya wafugaji ipo.
Anaweka mpango wa jinsi watavuka kipindi hicho na wanaufanyia kazi.
Siku moja usiku anaamshwa na mtu anayegonga mlango wake, anakuta ni mwanajeshi anamuulizia Mendel.
Wanajeshi walioenda kwenye mapambano wamerudi wachache wakiambatana na kanali Joll.
Wanataka chakula na mahitaji mengine, wanaenda kwenye ghala hakuna kitu. Wanamwambia Joll Mendel na wengine wameondoka na kila kitu.
Joll anakwepa, hataki kukutana na Hakimu.
Hakimu anamfuata na kumwambia kama kuna uadui kati yao wanapaswa kuumaliza baina yao na siyo kuumiza wengine.
Joll hamjibu anaamrisha wanajeshi alionao waondoke.
Hakimu anamkamata mmoja na kumwambia hatamwachia mpaka amwambie nini kimetokea.
Anamjibu wanajeshi wao wengi wamekufa kwa njaa na baridi, wafugaji waliwatega na kuwapeleka mpaka kwenye milima kisha kuwaacha hapo wakiteseka na kufa.
Kwa kifupi wameshindwa vita na wafugaji bila hata ya kupambana nao, bali wametumia uzoefu wao wa mazingira kuwashinda.
Hakimu anaendea kupata ndoto zake za mji uliofunikwa, anapoamka asubuhi anajikuta uume wake umesimama sana, inamchukua saa nzima kusubiri ulale.
Anajiambia ni muda mrefu hajafanya mapenzi, anaenda kwenye duka na kupewa dawa ya asili ya kuondoa hali hiyo.
Anamuuliza mwenye duka mbona duka lake halijaporwa na wanajeshi, anamjibu walimwambia hawana haja ya kulipora maana wafugaji wakija hawataliacha.
Muuza duka huyo anamwambia hakimu kwamba alizaliwa hapo na atafia hapo, wanaokuja wataondoka wamuache.
Hakimu anakutana na mmoja wa mabinti aliokuwa anatembea nao, ana mtoto mdogo, lakini anamshawishi akalale naye.

Analala naye kwa siku kadhaa, hana hisia zozote kwake, anaamua kuachana na hilo.
Anajaribu kukaa chini na kuandika historia ya kile kilichotokea, picha ya ndoto aliyokuwa anapata muda mrefu inamjia, huo ndiyo mji uliotelekezwa.

👉SOMO.
Riwaya hii ina mengi mno ya kutufundisha kuhusu umuhimu wa utawala unaofuata sheria na haki, madhara ya mipango ya utawala isiyozingatia uzoefu wa watu walio eneo husika na hata udhaifu binafsi wa mtu unavyoweza kutumika kuleta madhara makubwa.
Riwaya hii ina uhalisia mkubwa wa maisha yetu ya kila siku na hali tunazopitia, yapo mengi ya kujifunza.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,
www.t.me/somavitabutanzania